TANGAZO LA SERIKALI NA. 899 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMSHAURI YA WILAYA YA KARAGWE YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmshauri ya Wilaya ya Karagwe ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmshauri ya Wilaya ya Karagwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na mzigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au Wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmshauri ya Wilaya ya Karagwe;

"hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo ya bidhaa, kazi au huduma katika mwaka wa mapato;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kipindi maalumu cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara kwa Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo au soko lililotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

Sura ya 167

"hifadhi ya barabara" maana yake ni kama iliyoainishwa katika Sheria ya Barabara;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Ushuru wa Huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa au unaokusanywa na Halmashauri kutoka kwa Kampuni, tawi la Kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"ukokotoaji" maana yake ni namna ya kuandaa kiasi cha Ushuru wa huduma kitakacholipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

## SEHEMU YA PILI
## NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au wakala kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ushuru wa huduma

7.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na ushuru wa bidhaa kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii kutoka kwa wafanyabiashara wenye leseni za biashara ambao hawawasilishi hesabu za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(3) Kila mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye anawajibika kulipa ushuru wa huduma atalazimika kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa za hesabu za mwaka kwa ajili ya kukokotoa kiwango cha ushuru wa huduma.

(4) Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma kwa walipa ushuru wa huduma wanaowasilisha taarifa za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na walipa ushuru wa huduma katika kipindi maalumu cha hesabu.

(5) Mlipa ushuru wa huduma atatakiwa kulipa ushuru wa huduma si zaidi ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Halmashauri baada ya kupata idhini ya Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuuza mali za mdaiwa kwa njia ya mnada baada ya siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa.

(4) Halmashauri baada ya kupata kibali cha Mahakama itakuwa na uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa ambazo zinaweza kuharibika kwa haraka kabla hazijaharibika

(5) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika aya hii, Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, itatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala

Uteuzi wa wakala

9.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na
(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni

kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii

Makosa

11. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa au atadharau au atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; au

(f) atatumia chombo chochote kile kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu

iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa TS Na. 301 la Mwaka 2008

14. Sheria ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ya Mwaka 2008.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengezwa chini ya aya ya 4(1))*

### SEHEMU YA KWANZA: USHURU WA MAZAO

| Namba. | Aina ya mazao | Kiwango kwa Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Viazi | 3% ya bei ya kununulia. |
| 2. | Kabichi | 3% ya bei ya kununulia. |
| 3. | Karoti | 3% ya bei ya kununulia. |
| 4. | Matunda | 3% ya bei ya kununulia. |
| 5. | Vitunguu maji | 3% ya bei ya kununulia. |
| 6. | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia. |
| 7. | Mchele | 3% ya bei ya kununulia. |
| 8. | Mahindi/alizeti/mtama/mpunga | 3% ya bei ya kununulia. |
| 9. | Pamba | 3% ya bei ya kununulia. |
| 10. | Zao jingine lolote linalolimwa au kuuzwa katika Halmashaur | 3% ya bei ya kununulia. |
| 11. | Pumba | 3% ya bei ya kununulia. |
| 12. | mashudu | 3% ya bei ya kununulia. |
| 13. | Kibali cha kununua mazao | 50,000/= kwa Mwaka |

### SEHEMU YA PILI: USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA VYOMBO VYA USAFIRI AU BIASHARA

| Namba. | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki iliyosajiliwa kwa biashara | 500/= kwa siku |
| 2. | Teksi | 1000/= kwa siku |
| 3. | Lori lenye uzito chini ya tani 7 | 1,500/= kwa siku |
| 4. | Lori lenye uzito zaidi ya tani 7 | 2,500/= kwa siku. |
| 5. | Magari mengine yasiyo ya biashara | 500/= kwa siku. |
| 6. | Ushuru wa kituo cha mabasi au stendi: | |
| | a) Basi kubwa la abiria zaidi ya 30 | 3,000/= kwa siku |
| | b) Basi kubwa la abiria 20-30 | 2,000/= kwa siku |
| | c) Basi dogo | 1,000/= kwa siku |
| | d) Teksi | 1000/= kwa siku |
| | e) Pikipiki | 500/= kwa Siku |
| | f) Bajaji | 500/= kwa siku |
| | g) Gari nyingine | 500/= kwa siku |
| | h) Mtu | 200/= kwa mpito |

*Tangazo La Serikali Na. 899 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Ushuru wa maegesho ya vyombo vya majini kwa siku | |
| | a) Jahazi au ngama | 3,000/= |
| | b) Mtumbwi wa injini | 2,000/= |
| | c) Boti ya kawaida | 2,000/= |
| | d) Meli au feri | 5,000/= |
| 8. | Ushuru wa vituo vya kuoshea magari | 10,000/= |
| 9. | Kupakia na kushusha mizigo kwenye gari lenye uwezo wa kubeba chini ya tani 7 | 5,000/= |
| 10. | kupakia na kushusha mizigo kwenye gari lenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 7 | 10,000/= |

SEHEMU YA TATU: ADA AU USHURU WA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI AU MICHEZO AU BURUDANI

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha ngoma za jadi | 20,000/= kwa siku |
| 2. | Kibali cha kuchezesha disko au maonesho ya bendi au sanaa za maonesho | 20,000/= kwa siku |
| 3. | Kibali cha kuchezesha michezo ya bahati nasibu | 25,000/= kwa mwezi |
| 4. | Play Station | 80,000/= kwa Mwaka |
| 5. | Mechi ya mpira katika kiwanja cha Halmashauri au binafsi | 20,000/= kwa siku |
| 6. | pool table | 80,000/= kwa Mwaka |
| 7. | Kibali cha mechi ya mpira | 5,000/= kwa kila mechi |
| 8. | Mashine ya bonanza au Spot betting (slot machine) | 80,000/= kwa mwezi kwa kila mashine |
| 9. | Bonanza | 40,000/= kwa siku |
| 10. | Kibali cha uganga wa jadi | 40,000/= kwa Mwaka |
| 11. | Burudani za Taasisi au Kampuni | 20,000/= kwa tukio |
| 12. | Matangazo | 40,000/= kwa siku |
| 13. | Sherehe | 20,000/= kwa siku |
| 14. | Biashara ya muziki wa kompyuta | 20,000/= kwa Mwaka |
| 15. | Kumbi ya video au kibanda umiza | 40,000/= kwa Mwaka |
| 16. | Ushuru wa upambaji kumbi za sherehe na mikutano | 10,000/= - 20,000/= kwa siku/tukio |
| 17. | Kibali cha muziki Baa | 80,000/= kwa Mwaka |
| 18. | Kuendesha ligi | 50,000/= kwa ligi |

| | | |
|---|---|---|
| 19. | Duka la kazi za sanaa | 20,000/= kwa Mwaka |
| 20. | Marathoni | 50,000/= kwa tukio |
| 21. | Ushuru wa MC au DJ au Video Shooter | 10,000/= Kwa siku |
| 22. | Kituo cha mazoezi ya viungo | 50,000/= kwa Mwaka |

SEHEMU YA NNE: USHURU WA HUDUMA YA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA MABUCHA

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | ukaguzi wa nyama kwa kila ng'ombe atakayechinjwa | 5,000 |
| 2. | kuchinja mnyama kwa kila ng'ombe atakayechinjwa | 5,000 |
| 3. | Kuchinja na kukaguzi nyama kwa kila kondoo au mbuzi atakayechinjwa | 3,000/= |
| 4. | Kuchunja mnyama kwa kila nguruwe. | 5,000/= |
| 5. | Ushuru wa kulaza ng'ombe machinjioni | 3,000/= kwa siku kwa kila mmoja |
| 6. | kulaza mbuzi machinjioni | 1000/= kwa siku kwa kila mmoja |
| 7. | kulaza kondoo machinjioni | 500/= kwa siku kwa kila mmoja |
| 8. | Bucha ya Ng'ombe au Mbuzi au Nguruwe au Kondoo | 50,000/= kwa Mwaka |
| 9. | kuchanja mifugo | Kama itakavyopangwa na Serikali |

SEHEMU YA TANO: USHURU WA MINADA YA MIFUGO NA MAZAO YA MIFUGO

(Ulipwe na mnunuzi)

| Namba. | Aina ya Mfugo au zao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 5000/= kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi au Kondoo, | 1,500/= kwa kila mmoja |
| 3. | Kuku au kanga au bata | 3,000/= kwa kila tenga lenye kubeba 10-20 |
| 4. | Kuku au kanga au bata | 4,000/= kwa kila tenga lenye 21-30 |
| 5. | Punda | 3,000/= |
| 6. | Mikokoteni ya wanyama kazi | 20,000 kwa Mwaka |
| 7. | Ngozi za ng'ombe (1 hadi 50) kwa ajili ya biashara | 5,000/= |
| 7. | Ngozi za ng'ombe (51 hadi 100) | 10,000/= |
| 8. | Ngozi za ng'ombe ( 101 na zaidi) | 15,000/= |
| 9. | Ngozi za mbuzi au kondoo (1 hadi 50) | 2,500/= |
| 10. | Ngozi za mbuzi au kondoo (51 hadi 100) | 5,000/= |
| 11. | Ngozi za mbuzi au kondoo (101 na zaidi) | 7,500/= |
| 12. | Kusajili mkokoteni wa biashara | 30,000/= kwa Mwaka |

SEHEMU YA SITA: USHURU WA SAMAKI AU DAGAA MAZAO YAKE

| Namba. | Aina ya Samaki au Dagaa au Zao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Samaki | 100/= kwa kilo |
| 2. | Dagaa | 2,000 kwa gunia |
| 3. | Mabondo | 2% ya bei ya soko |
| 4. | Furu | 2,000 kwa gunia |

SEHEMU YA SABA: ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Namba. | Aina ya huduma | Kiwango kwa Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya vikao, mikutano na sherehe | 100,000/= hadi 1,000,000/= kwa siku |
| 2. | Kukodi viti vya Halmashauri | 500/= kwa kiti kimoja kwa siku |
| 3. | Mitambo (Grader, scavator, roller, trekta, lori,vifaa vya upimaji, n.k) | 50,000/= hadi 2,000,000 kwa siku |
| 4. | Kukodi vipaza sauti na matarumbeta | 100,000/= kwa siku |
| 5. | Kutumia uwanja wa michezo kwa shughuli za biashara | 20,000/=kwa siku |
| 6. | Kusoma nyaraka za wazi za Halmashauri | 500/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Kutumia maktaba ya Halmashauri | 500/= kwa siku |

SEHEMU YA NANE: ADA YA PANGO LA VIBANDA VYA BIASHARA AU NYUMBA AU OFISI ZA HALMASHAURI

| Namba. | Aina Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Vibanda vinavyozunguka stendi au soko na sehemu nyingine | Zitapangwa kutokana na bei ya Soko. |
| 2. | Nyumba za Halmashauri | a) Grade A 150,000/=<br>b) Grade B 80,000/=<br>c) Grade C 20,000/= |
| 3. | Ofisi za Halmashauri | Zitapangwa kutokana na bei ya Soko. |

SEHEMU YA TISA: USHURU WA SHUGHULI ZA MADINI

| Namba. | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mchanga au mawe ya madini kwenye kiroba chenye ujazo wa kilo 50 unaosafirishwa nje ya eneo la Uchimbaji/leseni | 1,000/= kwa kila mfuko |
| 2. | kila karasha | 10,000/= kwa mwezi |
| 3. | kila mwalo | 10,000/= kila mwezi |
| 4. | mfuko wa mchanga au mawe ya madini kwenye kiroba chenye uzito wa kilo 50 kutoka katika eneo la uchimbaji au eneo la leseni kwenda nje ya Halmashauri | 2,000/= kwa kila mfuko |
| 5. | Muuzaji wa marudio | 5% ya bei ya kuuzia |
| 6. | Makapi ya marudio | 5% ya bei ya kuuzia |
| 7. | Mpangishaji wa PML na mashamba | 5% ya bei ya kupangishia |
| 8. | VAT leaching Plant | 50,000/= kwa mwezi |
| 9. | Elution Plant | 60,000/=kila column (tenki lenye Carbon) |
| 10. | Wenye leseni za madini wanapaswa kuwajibika kwa jamii (CSR) | Kiasi kisichopungua 1% ya mapato yake kwa Mwaka |
| 11. | Usafirishaji wa mchanga wenye madini (marudio) | |
| | a) Uzito wa tani 1 – 9 | 21,000/= |
| | b) Uzito wa tani 10 – 15 | 30,000/= |

SEHEMU YA KUMI: USHURU WA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA GULIO AU SOKO AU MNADA

| Namba. | Aina ya gari | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari la mizigo lisilozidi $M^3$ 3 | 1,000/= kwa siku |
| 2. | Gari la mizigo linalozidi $M^3$ 3 | 2,000/= kwa siku |
| 3. | Magari mengine | 500/= kwa kila moja kwa siku |
| 4. | Kibali cha kununua na kusafirisha vyuma chakavu au plastiki | 10,000 kwa mwezi |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA: ADA YA UKAGUZI WA RAMANI YA UJENZI

| Namba. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | 0 hadi $50m^2$ | 10,000/= |
| 2 | 51 hadi $100m^2$ | 20,000/= |
| 3 | 101 hadi $150m^2$ | 40,000/= |
| 4 | 151 hadi $200m^2$ | 50,000/= |
| 5 | 201 hadi $250m^2$ | 75,000/= |
| 6 | 251 $m^2$ na zaidi | 200,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI: ADA YA VIBALI VYA UJENZI NA URASIMISHAJI WA VIWANJA

| Namba. | Aina ya Jengo au Kiwanja | Kiwango cha Ada kwa kibali (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kiwanja cha Makazi | 25,000/= |
| 2. | Kiwanja cha biashara | 50,000/= |
| 3. | Gorofa 1 | 200,000/= |
| 4. | Kiwanda au bohari au ghala | 200,000/= |
| 5. | kukagua kiwanjachenye ujazo mdogo | 10,000/= |
| 6. | Kiwanja cha Biashara na makazi | 70,000/= |
| 7. | kukagua kiwanja chenye ujazo wa kati | 20,000/= |
| 8. | kukagua kiwanja chenye ujazo mkubwa | 50,000/= |
| | kukagua kiwanja kikubwa zaidi | 70,000/= |
| 9. | kubadili matumizi ya jengo | Inategemea aina ya jengo |
| 10. | Kuzungusha mabati wakati wa kujenga | 500/= kwa mita moja |
| 11. | Maombi ya kiwanja | 20,000/= kwa fomu |
| 12. | Ujenzi wa mnara wa simu | 300,000/= |
| 13. | Mnara wa simu wenye booster | 2,500,000/= kwa Mwaka |
| 14. | Mnara wa simu usio na booster | 2,000,000/= kwa Mwaka |
| 15. | Ujenzi wa ukumbi wa sinema au mpira au starehe | 150,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 16. | Ujenzi wa uzio | 30,000/= |
| 17. | Ujenzi wa taasisi mbalimbali ambazo sio ghorofa | 150,000/= |
| 18. | Ujenzi wa kiwanda kikubwa | 500,000/= |
| 19. | Ujenzi wa Kiwanda cha kati au kidogo | 100,000/= |
| 20. | Ujenzi wa skimu ya uchenjuaji | 100,000/= |
| 21. | Ujenzi wa ghala au bohari | 100,000/= |
| 22. | Ujenzi wa jengo ambalo halijatajwa pamoja na marekebisho ya ujenzi | Inategemeana na aina ya jengo |
| 23. | Nukuu ya bei kwa kila fomu | 5,000/= |
| 24. | Ujenzi wa mwalo | 50,000/= |
| 25. | Kusimika karasha | 50,000/= |
| 26. | Ghala la kuhifadhia nafaka | 50,000/= kwa Mwaka |
| 27. | Ukaguzi wa mazingira ya ujenzi wa skimu ya uchenjuaji, Ilussion na CIP | 200,000/= |
| 28. | Kufanya ukaguzi wa mazingira ya eneo la ujenzi wa mwalo au karasha | 50,000/= |
| 29. | Kila ghorofa inayoongezeka kutoka ghorofa ya 1 | 100,000/= |
| 30. | Kubadilisha matumizi ya ardhi kutoka makazi kwenda biashara | 50,000/= |
| 31. | Kubadilisha matumizi ya ardhi ya Makazi kwenda viwanda | 100,000/= |
| 32. | Kubadilisha matumizi ya ardhi ya biashara kwenda makazi | 40,000/= |
| 33. | Kubadilisha matumizi ya ardhi ya Makazi au biashara au viwanda kwenda matumizi mengine | 100,000/= |
| 34. | Urasimishaji | 100,000/= kwa kila kiwanja isizidi 150,000/= |
| 35. | Kuzingira eneo au Jukwaa | 1,000/=kwa mita |
| 36. | Kodi ya jengo la kawaida | 10,000/= kwa kila jengo kwa Mwaka |
| 37. | Kodi ya ghorofa | 20,000/= kwa kila sakafu kwa Mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA TATU: USHURU WA MAZAO YA MISITU YA HALMASHAURI

| Namba. | Aina ya zao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gunia la mkaa | 5% ya bei kwa kila gunia |
| 2. | Nguzo za miti | 500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Lita 20 ya Asali | 2,000/= |
| 4. | Nta Kilo 1 | 100/= |
| 5. | Gogo | 2,000/= |
| 6. | Fito $M^3$ 1 | 6,500/= |
| 7. | mbao moja | 350/= |
| 8. | Banzi | 200/= |
| 9. | Kuni ujazo wa $M^3$ 1 | 6,500/= |
| | Kitanda cha mti wa kupandwa | 10,000/= |
| | Meza | 5,000/= |
| | Kiti | 2,000/- |
| | Flemu au topu za milango | 10,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NNE: USHURU YA MATANGAZO AU MABANGO KWA MWAKA

| Namba. | Aina ya Matangazo au Mabango | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Bango lisilo na mwanga | 15,000/= kwa futi ya mraba |
| 2. | Bango lenye mwanga | 18,000/= kwa futi ya mraba |
| 3. | Bango kwenye kuta | 10,000/= kwa futi ya mraba |
| 4. | Bango la kielektroniki | 20,000/= kwa futi ya mraba |
| 5. | Gari la matangazo | 10,000/= kwa futi moja ya mraba |
| 6. | Matangazo kwenye kituo cha mauzo:<br>i. Bango lisilo na mwanga<br>ii. Bango lenye mwanga | 10,000/= kwa futi moja ya mraba<br>20,000/= kwa futi moja ya mraba |
| 7. | Tangazo la bango linaloelekeza sehemu ya huduma ya kijamii inayopatikana katika Shule au Zahanati au Hospitali au sehemu nyingine | Hakuna Ushuru |

## JEDWALI LA PILI

## HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 13)*

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Karagwe, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya mwaka, 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU :
Jina:…………………………………..……………………
Saini………………………..………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutilia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Karagwe uliofanyika mnamo tarehe 24 mwezi Februry mwaka 2023 na kushuhudiwa lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

MICHAEL F. NZYUNGU
*Mkurugenzi wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe*

WALLACE M. MASHANDA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya karagwe*

NAKUBALI

Dodoma
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGELWA (MB)
*Waaziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikao Na Serikali za Mitaa*